Jarida La Kila Mwezi

# NGURUMO ya Mwandishi

Toleo La XVIII
Machi MMXXIII



## Kitabu ni Zawadi...

...mpatie mwanao!

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Kitabu ni Zawadi—Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Kelvin Kagambo— Uk 03

**New In Town—** Cronoc 7, Handaki la Panya, Shondwe la Mama Mkwe- 04

**PITIO LA VITABU**— MFADHILI—Uk 05

**MAKALA**— SAIKOLOJIA: —Mwamshe Huyo Wewe…Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Nilimuua Dada Niolewe Na Shemeji — uk 08 na 09

**MIAMBA WA AFRIKA:** Samora Machel (02) — Uk 10

**ANA KWA ANA**: Hannan Mzamba: Kutoka Loleza Seko' Mpaka Kona ya Riwaya Book Club-Uk 11

**RIWAYA:** Mpigambio—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7-Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: Sadiki na Chitemo—Uk 16

**HABARI/MATANGAZO**– Uk 17

SHUBAKA LA VITABU: Jinsi ya kutunza vitabu—Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** Kovu la Moyo — Uk 19

**MATANGAZO:** Uk 20

**NGURUMO YA MWANDISHI**

***©RICHARD MWAMBE***

**WASILIANA NASI**

**0766 974 865 AU 0672 160 016**

**WhatsApp: +255 734 550 514**

## TAHARIRI: Kitabu ni Zawadi…

Salaam kwenu nyote,

Ni tumaini langu mu bukheri wa afya, na Mola wetu bado anakupiganieni.

Basi, tunakusalimieni sana kutoka hapa chumba cha habari. Nikiwatazama naona kila mmoja anatabasamu kwa kuwa jarida limemfikia likiwa na kurasa za zaidi. Kazi yetu ni kujibu kilio chenu na kuikata kiu yenu.

Wakati ninapitapita mitaani na mitandaoni kusaka habari na mambo mengine, nimejikuta nikipigwa bumbuwazi na habari nyingi zinazosambaa siku hizi. Habari hizi zinafanya kila mzazi afungie ndani mwanawe kwa kuogopa wale wasio haya kuwa wanaweza kumharibu.

Watoto wa kiume wanaandamwa na wanaume wanapoteza uanaume wao kwa kile kinachoitwa ushoga na ndoa za jinsi moja. Hili ni janga, hata mimi nasema kuwa hili ni janga lazima kupambana nalo kwa nguvu zote ambazo Mwenyezi ametupatia. Kivipi? Hapa ndipo tunapokwama katika kufikiri. Ndugu zangu nachelea kusema kwamba janga hili ambalo linawaandama wanaume tumelifuga wenyewe kwa miaka mingi tu. Mabadiliko ya mitindo ya maisha katika familia zetu yamechangia parefu sana kufika hapa. Hatukuziba ufa, sasa tunajikuta tuna kazi ya kujenga ukuta. Kila mtu lawama kwa serikali. Tujiulize, serikali na wewe ni nani anayelea watoto ana kwa ana?

Basi kama tulikosea kwenye familia zetu, dawa ya janga ni kurekebisha kwenye familia zetu. Malezi! Tunu ya malezi kwa mtoto wa Kiafrika hususan wa Kitanzania imeshuka sana. Mtoto ana uhuru wa kutaka na kufanya anachotaka, eti ndiyo tunaona tumestaarabika. Tunapotea.

Mtoto anachezea simu janja ya ama ya baba au ya mama, anaachwa apekue anavyotaka. Humo sasa ndimo chanzo cha mengi kinapatikana. Wazazi tukumbuke kuwa watoto wa siku hizi siyo kama sisi wa miaka ile. Teknolijia ipo juu na watoto wetu wanakimbizana nayo. Kwanini mtoto tunampa vitu vizivyomfaa kama simu janja? Huko anapekua mitandao gani, anatazama nini, unajua? Ina maana wazazi hatujui mtoto anatakiwa apewe nini? Basi ngoja nikusaidie. Kama kweli tunahitaji watoto wetu wabadilike kimaadili basi mnyng'anye simu mpe kitabu. Kitabu ni zawadi inayofunguliwa mara kwa mara. Wape wanao vitabu kama zawadi kisha waambie wakimaliza kusoma wakusimulie na wakwambie walichosoma na kujifunza. Umewahi kujaribu? Kama bado jaribu sasa… nakwambia hivi utanishukuru baadae!

**© Ngurumo ya Mwandishi, Aprili 2023**

# MWANDISHI WETU: KELVIN KAGAMBO

**Naitwa Kelvin Donatus Kagambo,** nimezaliwa Dar es salaam Tanzania mwaka 1985. nimesoma mpaka Diploma. Elimu ya msingi nimesoma Karume, Dr. Omary zote za Mwembechai halafu nimesoma Kiwalani Shule ya Mwale na nipo nikamaliza darasa la saba. Sekondari nimesoma Chanika Sekondari. Baada ya kidato cha nne nikaenda kusoma DSJ ngazi ya cheti halafu Diploma miaka miwili.

Mimi naamini maisha yangu niliyokulia ndiyo yamenifanya kuwa mwandishi. Nimeishi na mama yangu tu wakati huo mama anafanya kazi ya mama ntilie. Alikuwa hawezi kuniacha peke yangu hivyo alikuwa ananichukua na kunipa pesa niende kuangalia filam kwenye banda maarufu la kwa Jangilaga, pale Magomeni Kagera.

Hiyo ilinifanya kuanza kupenda kwa sababu muvi ni *story telling* japo nilikuwa naona kama filam. Kutokana na na kwenda na mama eneo hilo kila siku nikaonekana kama mtoto wa stendi. Sasa pale stendi kulikuwa na watu wanauza magazeti. Nikawa napenda kusoma gazeti la sani hasa vikatuni. Lakini siku moja nilisoma hadithi ya Faki A. Faki inaitwa Maafa Makubwa. Niliposoma ile hadithi nikakuta nimependa sana nilichosoma. Nikaisoma sana mpaka ikaanza kunijengea matamanio ya kuanza kuandika. Basi nikaanza kuandika hadithi kama mtoto tu lakini pia nikaanza kusoma vitabu kama; Watoto wa Mama Ntilie, Takadini, nilivisoma nikiwa mdogo sikufikiri kama nitakutana navyo shuleni.

Nikajikuta naanza kuchanganya, nasoma sana, natazama sana muvi. Hivyo kusimulia stori ikawa ni kitu kilichoniingia sana. Sasa nikaja kuwa mwandishi kwa sababu, kwa mimi niliona naweza kufanya vyote yaani kuwa mwandishi na kuwa mtu wa filam. Lakini filam ni gharama huwezi kutengeneza peke yako wakati unachohitaji ni daftari na kalamu. Hivyo nilikuwa na daftari langu na ninalo mpaka leo.

Mimi mpaka sasa nimeandika miswada ya filam lakini pia nimeandika riwaya, zaidi kwa sasa hivi nafanya miswada ya filam, sijaandika riwaya kwa muda mrefu.  Lakini kwa kuipa exclusive Ngurumo ya Mwandishi, kwa sababu sina hata kitabu lakini nina plani ambayo niko nayo, nitakuja kuifanya kuhusu uandishi wangu wa riwaya. Kuna kitu ninakifanya, najaribu kukitengeneza, halafu nitakirudisha upande wa riwaya.

Uandishi wa riwaya na filam zote ni kusimulia stori. Tofauti ni kwenye uwasilishaji. Mimi nitakwambia filam ni ngumu sana zaidi ya riwaya kwa sababu kwa jinsi nilivyoandika riwaya au ninazozisoma naona ambavyo unaweza kuelezea mambo ya ndani ambayo anayo mhusika lakini kwenye filam ukifanya hivyo sana utaonekana we siyo mwandishi mzuri. Kwa hiyo utofauti ni uwasilishaji.

Riwaya ambazo nimeandika ni Mwanamke Kama Mama Yangu, Sauti Yake Masikioni Mwangu, Where Is My John?, Simu Ya Shemeji Mwajuma, Jamani Kei.

Na upande wa filam nimeandika na kuandaa; The Leaflet, Dogo, Naomba Eid Yangu, Chini Ya Chaga, Ubongo Kids, Akili And Me, Nuzo na Namia.

Kuhusu soko, kama unazungumzia malipo ya kifedha ni swala mtambuka. Lakini kuna film makers Tanzania wana pesa sana kupitia filam zao na kuna film makers Tanzania hawana hata pesa ya kula. Kuna waandishi Tanzania wanapata pesa sana kupitia uandishi wao na kuna waandishi hawana hata pesa ya kula. Kwa hiyo kwa mie naona ni swala mtambuka linalomtegemea mtu mwenyewe.


Penda kusoma vitabu

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini


Moja ya kitu ambacho nawaambia waandishi ni kuwa wawe wanaandika riwaya zilizo na DNA zao humo ndani. Tuwe na mitazamo isiyofanana na wengine.

Nawaambia Watanzania kuwa Tanzania imebarikiwa sana vipaji. Kwenye riwaya tuna waandishi wazuri sana sana sana. Kwenye filam tuna watengeneza filam wazuri sana sana sana. Mnatusapoti sana sana lakini wizi umekithiri. Sina darasa official la kufundisha uandishi wa filam lakini mtu akihitaji anaweza kunitafuta. Nipo Insta, facebook, tweeter

**By: Kelvin Kagambo**

## HANDAKI LA PANYA

**By: Kevin Mponda**

MUDA mfupi baada ya vijana wawili madalali wa jiji la Dar es salaam kubisha hodi ofisi za gazeti la FICHUA wakiwa na flashdisk yenye video ya tukio la kutisha, Jabu Kunambi, Mkurugenzi wa gazeti hilo anatekwa na kutoroshwa usiku wa manane.

Mfuko mweusi unapoondoshwa kichwani anajikuta kwenye bonde refu lililomezwa na msitu mnene wa kuogofya. Kutanabahi, mbele yake wamesimama watu aliopata kuandika habari zao gazetini. Anapofurukuta, kasiba ya bastola inamuonya. Kupiga kelele kusingefanya chochote mbele ya watu hao wasiojulikana.

Hii ni kazi mpya kabisa ya kijasusi iliyoingia mjini sasa. Mkono wa Jasusi Kevin Mponda, mwandishi mahiri wa riwaya za kijasusi na kipelelezi Tanzani.

Kamata sasa nakala yako kwa Kuwasiliana na mwandishi akupe maelekezo.

**Simu: 0688058669 / 0763382210 /0713419558**

## SHONDWE LA MAMA MKWE

**By: Mohamed H. Rajab**

SHONDE LA MAMA MKWE ni kitabu cha nne cha Mwandishi Mohammed Hammie Rajab.
Hii ni simulizi inayomhusu Kigenda Bakari, mke wa Akida. Mwanamke anayeamua kujifunga kibwebwe kupambania ndoa yake baada ya kuchoshwa na visa na vioja vya mkwewe.

Mkwewe, Bi. Mwanamtoo, alishajipanga. Visa, chuki, visirani, gubu na usihiri anavitumia kama silaha ya kujimilikisha nyumba anayolipa kodi mwanawe wa kumzaa.
Ni simulizi yenye visa vilivyofanyiwa tafiti, vinavyoakisi uhalisia wa maisha ya kila siku hasa kwa wakazi wa maeneo ya Pwani ambako ndipo hasa visa hivi vimezoeleka ijapokuwa vinaweza kutokea mahala popote.

Kitabu cha Shondwe ni mwendelezo wa ubunifu uitwao VISA VYENU aliowahi kuufanya baba yake Hammie Rajab wakati wa uhai wake. Simulizi zenye kuakisi maisha halisi ya ki"Tanzania.

Ukikihitaji kitabu hiki, wasiliana na mwandishi naye atakujuza jinsi gani utakipata

**Simu: 0653544133 / 0625634902**

## CRONOC 7

**By: Richard Mwambe**

Ni pale Nairobi mwanzo wa kila kitu. Mara tu baada ya vifo vya matajiri wawili huko Kenya, Kamanda Amata anajikuta katikati ya jambo lenye utata.

Utajiri wa Askofu Bariki Zebetoni nao unaleta mjadala serikalini na katika kanisa. Uchunguzi wa kina unafanyika lakini waneni wa kale walinena kwamba 'kikulacho ki nguoni mwako'.

Je mauaji ya matajiri hao wa Kenya na utajiri wa Askofu Bariki Zebetoni vina uhusiano wowote?

Jibu utalipata katika kitabu cha Cronoc 7.  ni kitabu kitamu cha kipelelezi kitakachokupa mafunzo na burudani. Ni mwandishi wako wa muda wote Richard Mwambe. Kukipata kitabu hiki wasiliana naye.

**Simu: 0682124486 / 0766974865**
**Whatsapp: 0672160016**

**Hakikisha unajipatia nakala laini za jarida lako la kifasihi nchini. Kila mwezi jarid hili linakujia tarehe 5;**

**Utalipataje? Wasiliana na wasambazaji wetu kama ifuatavyo, mawasiliano yote kwa WhatsApp**

**NGURUMO : +255 766974865, 0672160016**

# KITABU: MFADHILI –02



**Katika safu ya Pitio La Vitabu, leo tunaipitia riwaya ya MFADHILI iliyoandikwa na Hussein Issa Tuwa, na imepata cheti cha ithibati na kutumika mkwenye mtaala wa elimu ya sekondari.**

**Tahakiki hii inaletwa kwenu na Mwl. Furaha Venance**

**Tuendelee kuwachambua wahusika wakuu**

**2. Dania Theobald.**

Ø Ni binti wa miaka kama ishirini na nne.

Ø Ni binti mrembo na wakuvutia.

Ø Ni binti anayetoka katika familia ya kitajiri, kama mwandishi anavyothibitisha akimtumia muhusika Mama Mlole anaposema, " Akiwa ni mtoto aliyetoka katika familia ya Kitajiri." [Uk. 81]

Ø Ni msichana asiyedanganyika kwa fedha. Mwandishi anathibitisha hili akimtumia muhusika Mama Mlole anaposema, "Sio hivyo tu, bali Dania alikuwa ni binti mwenye uwezo kifedha; kwa hiyo hakuwa msichana aliyeweza kudanganyika kwa fedha kama wengine." [Uk. 82]

Ø Ni mwanamke anayehitaji penzi la kweli, rejea mwandishi anaposema "…hakuwa msichana aliyeweza kudanganyika kwa fedha kama wengine. Kwake kilichohitajika ni penzi tu." [Uk. 82]

Ø Mpenzi wa Jerry ambaye baadaaye anakuja kusalitiwa na Jerry kwa kuanza uhusiano na mwanamke wa Kizungu huko Marekani, kama mwandishi anavyosema akimtumia muhusika Mama Mallo, " Mwaka wa pili ulipoisha Jerry alileta barua kuwa alikuwa amepata mwanamke wa kizungu aliyepanga kufunga nae ndoa hukohuko Marekani." [Uk. 87]

Ø Alijaribu kujiua baada ya kusalitiwa na Jerry kama mwandishi anavyothibitisha akimtumia muhusika Mama Mallo anaposema, " …Sasa hili lilkuwa ni pigo la mwisho na Dania alivurugikiwa kabisa….alijaribu kujiua…" [Uk.87]


Ø Ni mama wa Junior aliyezaa na Jerry.

Ø Anaanza tabia ya ulevi wa kupindukia. Rejea mwandishi anaposema, "Alianza kunywa pombe kali tena kwa wingi." [Uk. 87] Pia katika Ukurasa wa 88 mwandishi anaendelea kuthibitisha hili anaposema, "Akawa mlevi wa kupindukia. Hakuna kilichomzuia kunywa pombe kali…"

Ø Anaanza uhusiano wa mapenzi na mwanaume mwingine aitwaye Gaddi Bullah baada ya kusalitiwa na Jerry.

Ø Anapata ugonjwa wa ini kutokana na athari ya pombe kali alizokuwa akinywa kama mwandishi anavyothibitisha akimtumia muhusika Dokta Virani anaposema, "Ini lake la kulia limeathirika kutokana na pombe kali alizokuwa akinywa, wakati wa mfadhaiko wake uliotokana na madhila aliyofanyiwa na Jerry." [Uk. 105]

Ø Anafadhiliwa sehemu/kipande cha ini na Gaddi Bullah ili lipandikizwe katika ini lake, mwandishi analithibitisha hili anaposema; "Gaddi Bullah ndiye mfadhiri wako Dania..." [Uk 140]




Ø Mapenzi yanaathiri utendaji wake kazini kwani hapo awali alikuwa ni mfanyakazi bora, mwenye nidhamu na ushirikiano kazini kama mwandishi anavyosema kupitia mhusika Mama Mlole; "Miaka minne iliyopita Dania Theobald alikuwa mmoja kati ya wafanyakazi wenye nidhamu, bidii na ushirikiano mkubwa hapa makao makuu." [Uk 81]

Baadhi ya tabia zake zinafaa kuigwa na jamii.

***Usikose sehemu ya mwisho***

# MWAMSHE HUYO WEWE, IGUNDUE NGUVU YAKO NA UITUMIE



**Neema Mgawo**

**Wataalamu wengi wa mambo ya Saikolojia wanakili kuwa ipo nguvu ndani yako ambayo unapoamua kuitumia inaweza kukupa matokeo chanya, nguvu hiyo ni ule uwezo ulionao ndani mwako.**

Kiuhalisia katika maisha yako au katika mwenendo wa maisha yako ya kila siku kuna ile namna ambayo kuna maneno unayasikia ndani mwako, yaani kuna ile hali unajikuta kama unajiongelesha, kama unajisemesha . Inaweza kuwa unajisemesha kwa kujionya au kwa kujipongeza, inaweza kuwa kwa kujisifia au kwa kujitahadhaharisha. Umewahi kutana na ile hali unataka kupita njia fulani lakini ghafra ukasikia sauti ndani yako ikikukataza kupita njia hiyo au ikakusisitiza kupita.

Sasa ile sauti inayotoka ndani mwako ni moja wapo ya wewe.
Labda hujanielewa, nisikilize, tulia halafu nisikilize, ikiwa hautoelewa basi mwisho wa hii mada nitaweka mawasiliano yangu, karibu nitakuelewesha.
Ni hiivi, kuna huo mwili wako ambao Mungu alikuumba, na kuna hiyo pumzi ambayo wakati unaumbwa Mungu alikupulizia(vitabu vya dini zote vinakili hivyo), kuna huo moyo wako unaodunda, kuna ubongo wako, na kuna hiyo sauti unayoisikia ndani mwako. Sasa, naposema  mwamshe huyo wewe aliye ndani mwako namaanisha iamshe hiyo nafsi yako ya ndani mwako. Iamshe hiyo nguvu ya ndani mwako na uitumie na ikusaidie. Igundue nguvu yako uliyonayo.

Mwamshe huyo wewe, aliyelala wakati maisha yako ni dhahiri kuwa hayaridhishi, una viungo vyote, unaweza kubuni kitu kikakuingizia kipato, hauna shida yoyote ya akili lakini kutwa kwenye mijadala ya kusema maisha magumu ilihali hauna juhudi zozote unafanya ili kujitafutia ridhiki. Mwamshe huyo wewe.

Mwamshe huyo wewe ambae kwa akili za kawaida umekata tamaa, hauoni kama mambo yako yanaenda, umejaribu kila namna lakini bado kila ukifurukuta haujioni ukipiga hatua, mwamshe huyo wewe ili uinuke upya na ubuni namna nyingine ya kwenda mbele. Sawa kwa njia hizo umeshindwa, basi amka upya, buni njia nyingine ili utoke kwa namna nyingine.

Mwamshe huyo wewe ambae unajihisi hatari na umekata tamaa, jitie nguvu upya inuka upya, anza upya.
Igundue nguvu ya ndani mwako na uitumie ili ikusaidie katika maisha yako ya kila siku, itumie nguvu hiyo kujiinua upya unapoanguka,
Itumie nguvu hiyo kujilinda wewe binafsi.
Itumie nguvu hiyo kujipenda.
Itumie nguvu hiyo kuishi maisha yako binafsi.
Itumie nguvu hiyo kufurahia maisha yako. Maisha ni haya sasa hivi unayoishi, yale ya baadae ni kwa kudra za Mungu hivyo jitahidi kufurahia maisha yako ya sasa.

Itumie nguvu hiyo kujiepusha na wale watakaoumiza hisia zako, nguvu hiyo isikilize pale inapokukanya kuhusu mwenendo na watu wakuzungukao.
Mwamshe huyo wewe, msikilize anaposema inuka uanze upya .

Igundue nguvu iliyopo ndani mwako na uitumie.
Igundue nguvu ya ndani mwako, jiamshe ili kufanya mambo kwenda kama unavyotamani. Ipo nguvu ndani yako ambayo ukiitafuta na ukaitumia sawasawa utanufaika nayo. Gundua uwezo wa kuendesha mambo ulionayo, gundua uwezo wako wa ziada na uutumie kukuletea matokeo chanya. Uwezo wako ukijiamsha unauona ukiwezesha kufanya nini? Mwamshe huyo wewe aliyendani mwako, iamshe hiyo nguvu iliyolala ndani mwako, usijihurumie katika kujiamsha, ruhusu maumivu ya

kujiamsha ili  kuwezesha ufanisi wa kazi ili kutimizia malengo yako.

Wakati unapojiamsha pengine kuna maumivu utayapitia, ndani ya moyo pengine kuna hali ya majuto utayapitia. Pengine unaamsha ule utu wako, ule ubinadamu wako wa ndani, maana kuna wakati ubinadamu huwa unapotea, sasa pengine muda unaojiamsha utapitia yale maumivu ya kujutia matendo uliyofanya, ruhusu kuumia ili uipate nguvu ya ndani uliyonayo. Igundue nguvu yako, itumie, mwamshe huyo wewe wa ndani ili akusaidie kuendesha mambo yako, akiendelea kulala  atafanya hata akili yako ione kila kitu ni kigumu kwako.

Madam Neema Mbilinyi Mgao: **0746 139 654**

***Igundue nguvu yako, itumie, mwamshe huyo wewe wa ndani ili akusaidie kuendesha mambo yako, akiendelea kulala  atafanya hata akili yako ione kila kitu ni kigumu kwako.***

Itumie nguvu hiyo kujilinda wewe binafsi.
Itumie nguvu hiyo kujipenda.
Itumie nguvu hiyo kuishi maisha yako binafsi.
Itumie nguvu hiyo kufurahia maisha yako.



# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI-03



**Mambo hayakuwa kama walivyodhani. Siku hiyo ilipita bila kumuona wala kuona dalili yake. Nyoyo zao ziliingia simanzi huku dada akijilaumu sana kwa kitendo chake cha jana.**

***Endelea***

Alijua huenda yule kijana alibadilisha njia hakutaka kuonana nao. Hakika ilikuwa ni majuto. Mwathirika mkubwa katika jambo hili alikuwa ni dada mwenyewe. Rafiki yake alijitahidi kumweka sawa ingawa ilikuwa kazi ngumu.

Siku ya pili nayo ilipita bila dalili ya kumuona yule kijana; siku ya tatu, ya nne. Wiki moja ilikatika. Wiki ya pili iliingia. Hakuna kijana wala dalili ya kijana. Unyonge ulirejea tena wakati huu ambao walidhani wamepata mtu wa kubadilishana mawazo na kucheka pamoja. Alijilaumu sana kwa hasira zake ambazo hakufahamu zilitokana na nini. Hakuamini kama kuulizwa swali lile ndiko kulisababisha kumwagia juisi.

Wiki mbili zilipita tangu tukio lile lilitokee. Hapakuwa na dalili za kumuona tena yule kijana. Kutokumuona kuliwapa ujasiri wa kumpigia simu. Bahati mbaya ikielekea upande wako haikwepeki. Katika siku zote walizojitahidi kumpigia simu hapakuwa hata na siku moja simu hiyo ilipatikana. Ilikuwa kama mkosi kwao. Kila walilopanga kulifanya lilikwama. Kwa hivi walijua wamemkosa na hawatomwona tena hata kwa bahati mbaya. Taratibu walianza kumsahau na kurudi katika maisha yao ya zamani – maisha ya kabla ya kumfahamu kijana yule.

Jumatatu moja wakiwa wamemsahau yule kijana, ghafla wakiwa katika mkao ule ule, dada alimuona yule kijana. Alitaka kukimbia. Alikwishachelewa. Yule kijana alishakaribia maeneo yao. Alikuwa anatoka kazini kwake kama kawaida. Alipowafikia alitabasamu. Kinyume na matarajio dada na rafiki yake waliinamia chini kwa wasiwasi.

"Jamani habari zenu?" Yule kijana aliwasalimia kwa utulivu.

"Salama tu. Habari za siku nyingi?" Aliitikia rafiki yake dada pekee.

"Njema kabisa. Habari za mjini hapa?" Bado dada hakuitikia. Alibaki kimya hadi yule kijana alipomshika kichwa na kumuinua ili amtazame usoni.

"We' vipi mbona uko hivyo, unaumwa?" Alimwuliza baada ya kuwa wametazamana kwa sekunde chache.
"Hapana siumwi," alijibu dada akirudisha kichwa chini.

"Kama huumwi mbona uko hivyo kulikoni?"
"Kawaida tu," alijibu dada.
"Haya kama ni kawaida," alisema yule kijana akitaka kuondoka. Wakati anataka kufanya hivyo dada na rafiki yake waliangaliana usoni halafu wakapeana kama ishara

"Tunaomba radhi kwa kilichotokea siku ile," rafiki yake dada alisema.

"Siku gani?" Aliuliza yule kijana.
"Siku ile tulipokuwa kwenye mapumziko ukaondoka ukiwa umechukia," rafiki yake dada alisema. Alikuwa msemaji mkuu.
"Aah! Yale mbona yalikwishaisha tangu siku ileile. Nyie bado mnayo tu hadi leo?" Yule kijana alirudi akaketi tena.

"Yeah! Tulijua umekasirika ukabadilisha na njia kabisa. Hukutaka kuonana na sisi tena."
"Nani amesema hivyo!" Kijana alishangaa.

"Tumeona tu vile ulivyotukimbia. Tulijua ni kwa sababu ya tukio lile."
"Hapana wapendwa. Si kama nilikasirika au kubadili njia ili nisionane na nyinyi. Mi' sikuwepo mjini hapa tangu Jumatatu iliyofuata baada ya tukio lile. Tulikuwa na project huko vijijini nami nilikuwa msimamizi. Nimerudi jana usiku. Si kama nilibadili njia."

Nyoyo za dada na rafiki yake zilifunguka zikaingia furaha.
"Msijali jamani yale ni mambo ya kawaida ambayo yanatokea. Yasiwape shida, yameshapita. Nadhani na Jumapili ijayo tutakwenda tena, au siyo?"
"Ha ha ha haaaaa! Haya."

"Ila wakati huu hatutokunywa juisi wala kuwa na chupa karibu yasije yakaibuka makubwa zaidi," alitania yule kijana. Walicheka. Walipoongea vya kutosha, yule kijana aliondoka kurudi kwake.

# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI—03

Dada na rafiki yake walifunga duka wakaondoka pia.

Uhusiano wao uliimarika zaidi. Dalili za mapenzi baina ya dada na yule kijana zilijionesha. Wakati huo majibu ya kidato cha sita yalikuwa yameshatoka, lakini hayakuwa mazuri kwa dada. Ila kwa yule kijana yalikuwa safi. Alifanya mpango wa kuomba chuo ambapo alichaguliwa kusoma shahada ya awali ya sayansi ya jamii katika chuo kikuu cha Dar es Salaam kwa udhamini wa shirika alilofanyia kazi. Hiyo haikumfanya yule kijana kupunguza upendo kwa dada. Alimpenda na kila siku penzi lao lilifana.

Nakumbuka, mara ya kwanza kumuona kijana huyu, ilikuwa wakati wa likizo ya kubadilisha darasa – kutoka kidato cha tano kuingia cha sita. Wakati huo alikuwa anajiandaa kwenda chuoni. Kweli dada yangu alikuwa na haki ya kupoteza network alipomuona kwa mara ya kwanza na kila alipomuona. Alikuwa kijana mpole lakini mcheshi, mwenye tabasamu murua aliyejawa na huruma.

Kuonesha dhamira haikuwa mbaya kwa dada, yule kijana alitoa taarifa kwao na baada ya makubaliano ya wanafamilia, walileta barua ya posa kwetu kumchumbia dada. Ilikuwa ni moja ya tukio ambalo siwezi kulisahau maishani mwangu. Nilikuwa namuona dada kila siku akizidi kuwa na furaha hasa tulipozungumza kuhusu yule kijana ambaye sasa alikuwa rasmi mchumba wake. Walitarajia kufunga ndoa muda wowote.
Sio siri, licha ya kumuona dada akifurahi niliingiwa na kinyongo na wivu. Sikujua vitu hivi vilitokea wapi na kwa nini. Nilitamani mimi niwe dada na dada awe mimi ili niipate ile nafasi ya kuolewa. Shemeji yangu alikuwa mzuri aliyenivutia hata nikajikuta nawalaumu wazazi wangu kunizaa baada ya dada. Nilijiambia kwa nini sikuzaliwa mimi halafu akazaliwa dada. Iliniuma sana kumuona dada akimpata kijana huyu mzuri na mtanashati.

Likizo ilipoisha nilirudi shuleni kuendelea na masomo. Niliingia kidato cha sita. Nilikwenda shuleni huku nikiwa na msongo wa mawazo. Mawazo hayo yalitokana na mahusiano ya dada na yule kijana ambaye ni shemeji yangu mtarajiwa. Unaweza kushangaa kwa nini badala ya kufurahia nilikasirika. Kitu kilichonikasirisha si dada kuolewa, la! Nilikasirika kwa nini aolewe na kijana mzuri kama yule ambaye hata mimi nilipomuona siku ya kwanza na kuambiwa kuwa ni shemeji yangu mtarajiwa, moyo wangu ulisimama kufanya kazi kwa sekunde kadhaa.
Sikutaka kijana huyu amuoe dada. Nilitaka anioe mimi. Pamoja na kuwa nilikuwa nasoma, kitendo cha dada kutaka kuolewa na huyu kijana kilinifanya na mimi nitamani kuolewa. Kibaya ni kwamba sikumtaka mtu mwingine zaidi ya mchumba wa dada. Sikuwa na uwezo wa kufanya jambo lolote. Nilisubiri hiyo ndoa ifike basi.

*** * ***

Wiki mbili baada ya kufungua Shule dada alikuja shuleni kunitembelea kama afanyavyo. Ujio huo haukuwa maalumu kwa ajili ya kunitembelea tu, bali ulikuwa na ujumbe mzito. Ujumbe ambao ulinifanya nidondoshe machozi mbele yake. Dada alishangaa akanihurumia. Nadhani kwa sababu ya mapenzi yake mazito kwangu. Pia kwa kudhani nimefurahi sana habari hiyo kiasi cha kushindwa kuzuia hisia zangu. Masikini kumbe usilolijua ni kiza kinene. Dada hakujua kilichomo moyoni mwangu wala hakufahamu maumivu niliyoyapata kwa taarifa yake kitakachotokea.

“Jamani mdogo wangu nimekumiss sana. Wiki mbili tu zimepita tangu uondoke nyumbani kuja shuleni lakini nimekukumbuka sana,” dada aliniambia mara tu baada ya kufika shuleni na kupewa ruhusa ya kuonana na mimi.

“Yaani hunishindi mimi. Umefanya jambo la maana kuja maana sijui ingalikuwaje. Vipi nyumbani wazima?” Nilimwambia kwa tabasamu.
“Wote wazima. Unasalimiwa na shemeji yako.”
“Ha ha ha haaa! Naye anasemaje mbona hukuja naye?”
“Amebanwa na mitihani. Watafunga chuo hivi karibuni.”
“Mwenyezi Mungu atamjaalia.”
“Aamina! Enhe vipi kitabu?”
“Kitabu kimeanza kwa mchakamchaka hadi naogopa.”

“Usiogope mdogo wangu. Ndiyo inavyokuwa. Mambo yatakuwa poa.”
“Nashukuru.”
“Sasa, mi’ nimekuja kukutembelea. Lakini kwa kuwa ni mtu muhimu sana kwangu, nimekuja kukupa taarifa. Unaweza kukisia ni taarifa gani?”
“Mh! Usinambie umepata mwaliko wa kwenda Uingereza au Nigeria!”

***Itaendelea***

# MIAMBA WA AFRIKA

## Samora Machel - 02

Kamanda wa ANC, J.B. Marks alivutiwa na kijana huyo wa Msumbiji. (kulingana na Joe Slovo) Akaamuwa kumwondoa mmoja wa waajiriwa wa ANC kwenye ndege ili kumwacha Samora Machel apate usafiri. Machel akasafiri kwa ndege hiyo mpaka Tanzania na kujiunga na wapiganaji wa FRELIMO waliokuwapo jijini Dar es Salaam.

Akiwa Dar es Salaam, Machel alijitolea kwa ajili ya utumishi wa kijeshi, na alikuwa mmoja wa kundi la pili la wapiganaji wa FRELIMO waliotumwa kwa mafunzo nchini Algeria. Huku Tanzania, Machel, aliwekwa kuwa msimamizi wa kambi ya mafunzo ya FRELIMO, iliyopo Kongwa. Mwezi wa Septemba, Tarehe 25, 1964, baada ya FRELIMO kuanzisha vita vya uhuru, Machel akapandishwa cheo na kuwa kamanda mkuu, na kulifanya jina lake kujulikana hasa katika eneo la Mashariki la jimbo kubwa la Niassa lililokuwa na wakaazi wachache. Alipanda vyeo haraka katika safu ya jeshi la msituni, FPLM, na kuwa mkuu wa jeshi mara baada ya kifo cha kamanda wake wa kwanza, Filipe Samuel Magaia, mnamo Oktoba 1966.



Mwanzilishi na rais wa kwanza wa FRELIMO, Eduardo Mondlane, aliuawa kwa bomu Februari 3, 1969. Makamu wake, Mchungaji Uria Simango, alitarajiwa kuchukua nafasi hiyo - lakini badala yake Kamati ya Utendaji ya FRELIMO ilimteua mshindi wa tatu wa nafasi hiyo. Nafasi hizo tatu ziliwajumuisha Simango, Machel na mzalendo mkongwe na mshairi Marcelino dos Santos. Punde si punde Simango alianza kuwashutumu viongozi wengine wa FRELIMO katika kijitabu alichoandika cha 'Gloomy Situation in Frelimo'. Kutokana na hilo, Simango alifukuzwa kutoka katika chama hicho cha ukombozi. Uchaguzi uliofanyika mwaka wa 1970, Machel akachaguliwa kama Rais wa FRELIMO, na Dos Santos kama Naibu Rais.

Kama marehemu Mondlane, Machel alijitambulisha kuwa ni mfuasi wa falsafa za Umaksi-Leninism, na chini ya uongozi wake nyadhifa hizi zikawa muhimu kwa FRELIMO, ambayo iliibuka kutoka kwa mtazamo mpana uliozoeleka na kuwa chama cha Kimaksi zaidi.

Kamanda mpya wa jeshi la Ureno nchini Msumbiji, Jenerali Kaúlza de Arriaga, alijigamba kwamba angeiondosha FRELIMO katika muda wa miezi michache. Alianzisha mashambulizi makubwa zaidi ya vita vya kikoloni vya Ureno, Operesheni Gordian Knot, mwaka huo wa 1970, akiilenga Cabo Delgado iliyokuwa kama kitovu cha FRELIMO huko Kaskazini mwa Msumbiji. Kaúlza de Arriaga alijivunia kuharibu idadi kubwa ya vituo vya wapiganaji wa msituni - lakini kwa vile kambi kama yenyewe ilikuwa tu ni mkusanyiko wa vibanda, ushindi wa kijeshi kama huo ulitia shaka. Machel alijibu kwa kubadili mwelekeo wa vita mahali pengine, na kuongeza shughuli za FRELIMO katika jimbo la magharibi la Tete. Hapa ndipo bwawa kubwa lilikuwa linajengwa huko Cahora Bassa, kando ya Zambezi, ili kuuza umeme kwa Afrika Kusini. Kwa kuhofia kwamba FRELIMO ingeshambulia eneo la bwawa, Wareno waliweka safu tatu za ulinzi karibu na Cahora Bassa. Hili liliwanyima nafasi wanajeshi wengine wa mkoa wa Tete. Mwaka 1972 FRELIMO ilivuka Zambezi, ikipiga zaidi Kusini. Kufikia 1973, vitengo vya FRELIMO vilikuwa vikifanya kazi katika Manica na Mkoa wa Sofala na vilianza kugonga reli kutoka Rhodesia hadi Beira, na kusababisha hofu miongoni mwa walowezi wa Beira, ambao walishutumu jeshi la Ureno kwa kutofanya vya kutosha kutetea masilahi ya Wazungu. ***Itaendelea...***

# HANNAN MZAMBA: Kutoka Loleza Seko' mpaka Kona ya Riwaya Book Club

**Leo katika safu yetu ya Ana kwa Ana nimekutana na mwanadada mrembo, mcheshi na mwenye maneno mengi sana.**

**Mwanadada huyu ilinibidi kumtafuta baada ya kusikia habari zake kuwa ni muasisi wa Kilabu cha wasoma vitabu 'Book Club' cha Kona ya Riwaya. Nikaona isiwe tabu hebu atuambie mawili matatu kujihusu na kuhusu hilo afanyalo. Karibu!**

Naitwa Hannan NZAMBA
Ni mtoto wa nne kwenye familia yetu yenye watoto 6. Mimi ni mama wa watoto watatu. Mi nimezaliwa hapahapa Dar es salaam huko Ada Estate.

Shule ya msingi nimesoma Mbuyuni na sekondari nimesoma Loleza Mbeya. Mimi ni mjasiliamali ninayefanya shughuli zangu ndogo ndogo za kuniingizia kipato

Mimi katika maisha yangu nilipenda sana kuwa Pilot. Wala sikutaka kuwa mwandishi ila ni mapenzi yangu tu kwa vitabu ndiyo yaliyoleta wazo la kuanzisha hii Book Club.
Kilichonisukuma ni mapenzi kwa vitabu.

Chimbuko la kila kitu ni Loleza Secondary, pale alikuwapo mwalimu anaitwa Mwl. Mwakasege alikuwa ni mwalimu mzuri sana wa Kiswahili (Sijui kama yupo hai au la…). Yeye ndiye aliyenifundisha haya mambo ya uchambuzi wa vitabu. Kila nikifunga shule ananipa kitabu niende nacho nyumbani na shule ikifunguliwa nije nimwelezee kuhusu kitabu hicho.

Bado sijaona matokeo kwa sababu ndio kwanza tunaanza. Ila malengo yangu ni watu wapende kusoma vitabu. Mi naamini kuna mambo mengi sana ya kujifunza kwenye vitabu. Hata mwanao utamfundisha kusoma na akipenda kusoma, thamani ya vitabu itaonekana.

Mpaka sasa tumeshafanya uchambuzi wa vitabu kama cha;

- Adam Shaffi - mtoto wa mama
- Laura Pettie- kiroba cheusi
- Fadhil Mtanga - Fungate
- Mfadhili - Hussein Tuwa
- Ibrahim Gama- barua kutoka jela
- Hussein Molito - Chawa
- Maundu Mwingizi -
- Kitanda cha kuwadi
- Frank Masai - Mwimbula

Bado tunaendelea na mikutano yetu ya uchambuzi hivyo tunapenda kuwaalika watu wafike kwa wingi tujifunze kupitia chambuzi hizi.

Asante sana ndugu mwandishi



# MPIGA MBIO — 18



Richard Mwambe

**"Hapana nini? Wewe una mwanamke… na nilishawaambia dawa niliyowapa hutakiwi kuwa na mwanamke wa kudumu. Yaani wewe ukiwa na shida zako utafute, umalize, uondoke… usiwekeze!" Ngoreko alikasirika.**

**Endelea...**
"Mzee ni kweli, lakini Mimi sijafanya chochote na huyo mwanamke, na ulituambia kuwa kama mmoja wetu anapata mchumba basi amlete aogeshwe kwanza…" Kenneth akaeleza.

"Naaam!"
"Lakini Mimi bado, nilipanga nimlete…" akajitetea.
"Hahahahahaaaaaaaa…. Sikiliza kijana… penzi ni upofu, na penzi no kitovu cha uzembe…. Nakuona unakoelekea aua anakokupeleka huyu mwanamke, Ikunda…." Ngoleko akamtaja kwa jina. Wakiwa katikati ya Yale mazungumzo, simu ya Kenneth ikaita kwa fujo, akaichukua na kuitazama kiooni, Ikunda. Apokee asipokee? Akaitazama tena na kumtazama yule Mzee aliyemkazia macho. Akataka kuikata.

"Usiikate, pokea umsikilize, Ikunda anapiga simu…" Ngoleko aliongea kana kwamba aliona kuwa mpigaji ni Ikunda. Kenneth kwa kitetemeshi, akaiinua na kuiweka sikioni. Akaita Mara tatu na kutulia kidogo. Ile simu ikakatwa.

"Kuna nini?"Kebby akamuuliza Kenneth. Kenneth hakujibu, aliinuka na kuinama kumuelekea Mzee Ngoleko. Mzee yule akamchapa na usinga kichwani, "mje wote keso baada ya Maghalibi!" akatamka. Kenny akatoka nje ya ile nyumba na kufuatiwa na Kebby.

Nje ya ile nyumba Kenneth hakujua nini anapaswa kufanya. Kilanalipopiga simu ya Ikunda haikupokelewa. Akachanganyikiwa.

"Vipi brother…." akauliza Kebby.
"Kuna shida Kebby…"
"Wapi?"
"Sijui…"
Kenneth akavuta hatua za haraka mpaka kwenye kituo cha pikipiki, akachukua moja aliyoiona inafaa.
"Dogo nimepeleke Makumbusho…" akamwambia. Yule dogo hakuwa na hiyana, alipiga gia na kuitimua pikipiki ile kama imeibwa.

Dakika kumi na moja aliwasili nyumbani kwa Ikunda kwa miguu, baaa ya kuaicha ile pikipiki. Alipofika mlango ulikuwa umefunga, majirani wakamwambia kuwa Ikunda alitoka na rafiki yake. Ndipo akili ikamrudia kuwa Ikunda alimwambia kuwa yupo na Prisca. Bahati nzuri, namba ya mwanamke huyo alikuwa nayo. Akaipiga ikaita, akaiweka sikioni kusubiri mwitikio.

*** *** ***

Prisca akiwa nje ya ile baa simu yake ikaita, 'Mpiga Mbio' ilijiandika. Moyo wa Prisca ukaanza kudunda bila mpangilio. Hakuelewa tu imekuwa kijana huyo ampigie yeye. Prisca alijiuliza Kenneth kaipata wapi namba yake. Alishasahau kuwa miezi kadhaa nyuma alikuwa na mpango wa kumnasa kijana huyo, ni yeye aliyemwalika kule Slip Way kwa kinuwaji cha jioni, Kenneth alilikataa ombi LA mwanamke huyo. Kiapo! Alikumbuka kiapo.

Prisca akajitafakari afanyeje, Kenny anapiga simu kutoka wapi?

Lilikuwa swali gumu. Nipokee au nisipokee? Anajua kama Niko na Ikunda? Akabaki njia panda.

Simu ikaendelea kuita na kukatika, ikaanza kuita tena. Prisca alijikuta anapata baridi ilhali joto la Dar lilitamalaki, akahisi mkojo lakini hakukojoa. Nimefanya nini? Akajiuliza. Ikunda atanielewa kweli? Uongo gani nitamwambia? Maswali yakazidi kumiminika kama mvua zamasika. Majuto ni mjukuu, wahenga walisema na maji yakimwagika hayazoleki. Misemo onyo yote ya wahenga, Prisca aliikumbuka. Simu yake ikaita tena, akaitazama. Mpigaji ni yuleyule aliyemsevu kwa jina la Mpiga Mbio. Kenneth! Akawaza.

Mara hii akaikuta anaipokea simu na kuiweka sikioni pasi na kujua nini cha kujibu.
"Prisca! Upo wapi na Ikunda?" Kenneth akauliza kwa ukali. Sauti iliyopenya mpaka kwenye nyayo za mwanamke huyo. Akatulia kwa muda kabla hajajibu. "Si nakuuliza wewe?" Kenneth alizidi kufoka. Prisca akapata ujasiri ghafl, "kwani mi ni mlinzi wa Ikunda?" akasonya. "Mi sijaonana na Ikunda leo, na tangu lini mi nina urafiki na huyo

# MPIGA MBIO — 18



www.richardmwambe.com JAMVI la SIMULIZI

kidudu mtu! Sema tu kama unataka kuogea na mimi…" Prisca akamjibu Kenneth.
"Ikunda amenipigia simu amenambia yupo na wewe… na simu ya mwisho aliyopiga hakuweza kuongea kitu inaonekana yuipo kwenye hali mbaya…"
"Sawa! Lakini mi nimemrudisha mpaka kwake muda mrefu…" Prisca akajikanyaga.

"Prisca, tuheshimiane, si unesema hukuwa na Ikunda wewe…. Sasa mbona unasema umemrudisha? Hivi unanifanya bwege! Haya nambie Ikunda yupo wapi na wewe mwenyewe sasa hivi upo wapi?" Akamtupia mswali mfululizo. Prisca aligundua kosa alilofanya, alishindwa kusimama na uongo wake. Angefanyaje sasa?
"Nimemrudisha bwana, mi nipo zangu Sokoni Baa nakula maisha…" akajibu kwa hasira pasi na kujua keshaeleza mpaka mahali alipo.

"Mimi nipo nyumbani kwa Ikunda na majirani wanasema umeondoka naye hamjarudi…"
"Niache bwana!" Prisca akang'aka na kukata simu.

*** *** ***

Kenneth aliitazama simu yake, imekatwa. Akashikwa na hasira, akaitia mfukoni.
'Oya mzigo tayari huu!' sauti hii ikamrudia Kenneth, ikazidi kumtia machungu. Hii sauti ya Prisca kabisa! Akawaza na kufuata kijiwe cha bodaboda.
"Nipeleke Sokoni Bar" akamwambia dereva.
"Iko wapi hiyo?" Yule kijana akamuuliza.

"Mwenge nyuma tu ya jengo la Nakiete" akamwelekeza. Safari ikaanza. Haikuwachukua muda kwani kutoka Makumbusho alikokuwa akiishi Ikunda mpaka Mwenge ni pafupi sana.

Sokoni Bar ilisheheni watu muda huo. Kenneth aliposhuka kwenye pikipiki kwanza akatulia kutembeza macho huku na kule kuona kama kuna anayemjua au la. Afanaaleki! Macho yake yakalitambua gari La Prisca. Analijua, kwani ndilo lilimrudisha kutoka Slipway siku ya miadi yao. Alilikariri namba kwa haraka sana. Ilikuwa ni moja ya kazi yake kukariri mamba za magari na sura za watu. Akaliendea. Bahati nzuri, Prisca bado alikuwa nje akiongea na simu. Kenneth akamwona. Hakumshtua bali alimsogelea kwa ukimya kama jini.


'kwani shida nini? Hujamaliza tu'….'kitu gani? Unanifelisha Habibu tumia kazi yako atafyata tu….' Kenneth alisikia maneno hayo akajua, kumbe upande wa pili Luna Habibu. Kenneth alimjua Habibu vizuri tu kwani Nate alikuwa polisi mhalifu, mpenda rushwa na mtumia nguvu. Kawaida ya watu wanaofanya kazi kama ya Kenneth huwajua wahalifu wenzao wore wawe ndani au nje ya jeshi la polisi. Akamfuata Prisca na kuibuka mbele yake kama mzimu.

Prisca alijikuta anapigwa bumbuwazi, simu ikamwanguka, akatetemeka.
"We vipi? Ndo nini kufuatana kwenye starehe bwana? We si ulinikataa mimi, si ukinikataa… acha wanaume wenzio wafaidi…" Prisca akafoka huku akiokota simu yake.
"Usinijazie watu hapa!" akamalizia. Kenneth aliuma meno kwa hasira,

"Ikunda yuko wapi? Nijibu tu nikuache, ukinidanganya leo hutolala…"
"Khaaa… mi sikuwa na Ikun…."
"Unanijua vizuri? Mimi ndiyo Kenneth… kama ulikuwa hunijui, kesho utasimulia wenzio ukiwa tayari hauna Jicho moja…. Nambie Ikunda yuko wapi?"

"Bwana mi siju…" Prisca hakumaliza, akapokea Kofi moja zito LA mkono wa kulia. Akahizi kama kapigwa na kitu kizito shavuni. "Nambie, Ikunda yuko wapi? Usinifanye bwege!" Kenneth alifura kwa hasira. Prisca alipomtazama mwanaume huyo usoni alikutana na macho Makalu mithili ya nyoka, mshavu yaliyojaa gadhabu, akajua yupo kwenye hali ngumu.
"Unanidanganya? Haya sikiliza hii…" Simu ya Kenny kwa jinsi alivyoseti huwa inarekodi miito yote halafu usiku huwa anafuta ile asiyoitaka, na ile anayoitaka huiacha.

Akachukua simu yake na kuowasha sehmu ya kuhifadhi miito iliyorekodiwa. Akatafuta mwito was mwisho wa Ikunda, akamsikilizisha.
'Oya mzigo tayari huu'
'Haina shida niachie mimi, hapa wanajua shughuli zangu…'
Prisca alijikuta anaishiwa nguvu, kukataa hawezi kukubali hawezi.
***Itaendelea...***




SURA YA 01

**KILIKUWA chumba kilichojawa giza ambapo sauti za watu wawili tu zilikuwa zikisikika. Ilikuwa aina fulani ya kikao cha siri ambacho hakuruhusiwa mtu mwingine kuingia. Kila mmoja hakumwona mwenzake isipokuwa alisikia tu sauti ya mazungumzo yake.**

"Unanihakikishia kuwa kesho nitasikia kitu?" mmoja aliuliza.
"Bila shaka, maadam nimefika nitaifanya kazi vyema, lakini mpango ni uleule," yule mwingine alisikika akimjibu huyo aliyeuliza.
"Mmmm, ok! Sasa kama nilivyokwambia, kila kitu utakikuta kule hotelini, hakikisha unakamilisha mapema kwani ni swala lisilotakiwa uzembe, uzembe wako ni mauti yako".

"Yeah! Nimekuelewa, aliyekuunganisha nami anajua uwezo wangu, na nina uhakika hata wewe utaukubali,"
"Good! Kazi njema," wakaagana. Kilichofuata hapo ilikuwa ni sauti tu ya mlango ukifungwa upande ule wa pili na mara taa kali zikawaka. Taa zile zilimfanya yule mtu aliyebakia kufinya macho na kisha tarataibu kuyafunbua na kujikuta hayuko peke yake. Aliangaza macho huku na kule akawaona watu wengine watatu; wawili wanaume waliojazia vyema vifua vyao wakiwa wamevalia suti safi nyeusi na mmoja mwanamke aliyezibana nywele zake kisogoni, mrefu lakini si mwembamba sana. Mwonekano wake ulionesha kuwa ni mwanamke mjanja na asiyeogopa kitu. Naye alivaa suti nyeusi ya kiume iliyomkaa vyema mwilini mwake.

"Mwandaeni…" akawaambia wale vijana nao wakatoa soksi jeusi na kumvika kichwani. Wakamfunika uso. Kisha wakamkamata huku na huku na kumtoa ndani ya lile eneo. Hakuleta tabu kwani alijua wazi kuwa hiyo ndiyo njia ya kuingia na kutoka katika eneo hilo, maana ndivyo alivyoletwa.

*** *** ***

Subaru Forester jekundu lilikunja kulia na kuiacha barabara ya kwenda Nakuru. Likapita katika barabara mbovumbovu, katikati ya majengo kadhaa ya ghorofa. Baada ya majumba kama manne hivi lilisimama mbele ya jumba moja la ghorofa tano kwenye eneo la Westland jijini Nairobi.
'Piiiii! Piiiii!' honi ya gari hilo ilipigwa mbele tu ya lango kubwa lililo upande wa nyuma wa jengo lile. Punde tu lile lango likafunguka taratibu lakini aliyelifungua hakuonekana. lile gari likaingia ndani ya wigo na kupotelea uvunguni mwa lile jengo ambapo palikuwa na maegesho ya magari ya wateja. Milango ikafunguliwa, vijana wale wawili wenye suti wakateremka na kumfungulia mlango mtu wao. Yule mwanadada aliyekuwa nyuma ya usukani akashuka pia na kusimama nje.

"Tumefika!" akawaambia na wale jamaa wakamtoa lile soksi usoni na kijana huyo akawa huru.
"Nifuate!" yule mwanamke akamwambia. Naye akamfuata nyuma wakati yule mwanadada akiwa mbele. Baada ya kukwea ngazi kadhaa waliibukia ndani ya jengo lile. Akafungua mlango na kuingia mahali palipoonekana kama sehemu ya kumpumzikia palipokuwa na makochi kadhaa na meza ndogo iliyotengenezwa kwa kioo kizito juu na chini kulikuwa na sanamu ya mfano wa nge mkubwa aliyekibeba kile kioo cha juu kwa mkia wake.
"301," akamwambia mhudumu naye akamkabidhi funguo yule dada. Wakafuatana mpaka kwenye mlango wa chumba hicho.

"Una saa arobaini na nane tu za kumaliza kazi," akamwambia yule mtu. Hakujibu kitu zaidi ya kutikisa kichwa tu na yule mwanadada akaondoka zake. Ndani ya chumba hicho kulikuwa na kitanda kimoja kikubwa, meza ndogo na sofa moja la kutosha mtu mmoja. Yule mtu akavua koti lake na kulitupa kitandani. Kisha akaliendea jokofu dogo lililowekwa kwenye kona ya chumba hicho, alipofungua akatoa chupa kubwa ya pombe na kuiondoa kizibo. Hakuhitaji bilauri. Akapiga tarumbeta mafunda mawili ya haraka na kuirudisha.

Kabla hajafanya lingine lolote mlango wake ukagongwa. Akasita kidogo, lakini hakuwa na wasiwasi. Alipofungua mlango akagongana macho na mwanadada mweusi wa rangi, mfupi aliyejaa mwili, mapaja

yake yaliyojaa nyama yalionekana kukaa vyema ndani ya suruali aliyoivaa.
"Mzigo wako!" Yule mwanadada akamwambia huyo kijana. Naye akaupokea.
"Hili tu au kuna jingine?" yule mgeni akauliza.
"Hilo tu…"
"Asante!" Yule mgeni akajibu na kumsindikiza mwanadada huyo kwa macho.

*Mungu fundi!* Akawaza na kuurudisha mlango. Akiwa ameketi juu ya kitanda, alilifungua kasha lile dogo na ndani yake kulikuwa na bahasha. Akaichana na kutoa picha mbili zilizowekwa pamoja. Akaichukua ya kwanza na kuiangalia kwa makini. Ilikuwa picha ya mwanaume. Alikuwa ni Muindi, mnene na shingo yake ilipambwa kwa mkufu mzito wa dhahabu. Akaigeuza nyuma ile picha, ilikuwa nyeupe tu kama ilivyo picha nyingine zote. Akachomoa ya pili, nayo ilikuwa ya mwanaume, Mwafrika. Kwa kumtazama alikuwa na umri kati ya miaka hamsini na hamsini na tano hivi. Akazitazama zile picha kama zina uwiano wowote. Haikuwa hivyo. Alipokung'uta ile bahasha kikadondoka kidubwasha kidogo, ambapo alipokiona tu alijua ni cha kazi gani. Akakiokota na kukipachika sikioni. Hakikuwa kikubwa, bali kidogo kama punje ya indi, akabofya kitufeche na kusikilizia ujumbe uliomo.

"…Mr. Colbas, picha namba moja ni ya Zuganji Kumeil, anapatikana huko North Kinangop, anaishi katika jumba lake kubwa lililotengwa na mji kabisa. Ana wafanyakazi wasiopungua hamsini ndani na nje ya jumba lake. Kuingia katika jumba hilo unatakiwa kutumia akili ya ziada. Mtu huyu anatakiwa kuuawa bila kuulizwa swali lolote…"
Alipomaliza kusikiliza hayo akaiweka pembeni ile picha, mara akasikia sauti ya toni ikishiria kuna ujumbe mwingine.
"…Mr. Colbas, picha ya pili ni Bwana Patrick Njuwe, yeye anapatikana Mombasa, nyumba yake kubwa na ya kisasa inapatikana katika mwambao wa bahari opposite na Mombasa Resort, anatakiwa kuuawa bila kuulizwa swali. Lakini hivi tunavyoongea yupo Nairobi amefikia katika hoteli ya Casablanca. Unaweza kutekeleza jambo hilo hapohapo au Mombasa. Hakikisha unafuata maelekezo kama utakavyokuwa unayapata. Kumbuka una saa arobaini na nane tu kukamilisha hayo mauaji…kazi njema sana!"
Ile sauti ikakatika na hakukuwa na nafasi ya kuuliza swali wala kuulizwa. Akakichomoa kile kidubwasha chake na kukirudisha bahashani. Akavua saa yake pamoja na vikorokoro vingine vilivyo mwilini mwake. Akaingia maliwato kujiweka sawa tayari kwa kibarua alichopewa. Huyu aliitwa Colbas yaani Colman Basile, muuaji hatari wa kukodi, mara hii alikuwa katika jiji la Nairobi.

*** *** ***

North Kinangop, kitongoji kilichojitenga upande wa kulia wa barabara kuu ielekeayo Uganda. Kitongoji hichi kilichokaliwa na mabwanyenye wachache kilitoa picha halisi ya maisha ya watu wa nchi hiyo. Zuganji alipenda kuishi eneo hilo kutokana na hali ya hewa ya baridi na kuepuka muingiliano na makazi ya watu wengine. Alikuwa mtu mwenye ukwasi wa mali, pesa nyingi mpaka alishindwa kupanga matumizi yake.

Toyota Hilux liliegeshwa nyuma ya jumba la kisasa lililojengwa katikati ya shamba kubwa. Umbali wa kutoka katika jumba hilo mpaka ile ya jirani ilikuwa kama kilomita moja au moja na nusu hivi. Ukiangalia kwa macho ya haraka haraka utajua tu kuwa waishio hapo wote ni mabepari maana hakuna kumsalimia mwingine wala kuombana chumvi. Maisha ya Uswahilini, weka kando.

Mlango wa gari ukafunguliwa na kijana mmoja aliyevalia nadhifu kabisa akateremka na kuufungua mlango wa pili. Mtu mmoja, mnene, mweupe, mwenye nywele ndefu zilizomwagika mabegani akateremka. Mustachi wake ulimea vyema chini ya pua yake. Akiwa anatembea kwa msaada wa fimbo akavuta hatua huku akisindikizwa na kijana yule mpaka ndani ya lile kasri. Sebule kubwa iliyosheheni kila kitu ilimlaki, naye akajibwaga juu ya kochi mojawapo. Mtumishi wa ndani aliyejua wajibu wake akamletea kinywaji haraka.

"Niitie Morio," akamwambia mtumishi wake na yule mwanadada akaondoka zake na baadaye akaja kijana mmoja, mkubwa kwa umbo, akaingia na kusimama mbele ya tajiri huyo.
"Yes Sir!" akaitika.
"Keti," akamwambia.
"Sikiliza Morio, nimetoka mjini kwenye ishu muhimu, hali si shwari sana. Imegundulika kuna mchezo mchafu unatunyemelea. ***ITAENDELEA***

## SADIKI NA CHITEMO

**SADIKI ni mtoto anayeishi karibu na Ujiji. Anaye ndugu yake aitwaye Sikiri. Sadiki na Sikiri husoma katika shule ya #Businde. Sadiki anafanya kazi zote kwa bidii. Lakini Sikiri ni mtoto mbaya kwa sababu ni mvivu, kaidi, tena hana adabu.**

Siku moja wakati wa livu baba yao aliwaamsha mapema sana. Akasema, "Sadiki, chuukua hii shilingi. Nenda sokoni ukanunue samaki. Na wewe Sikiri, nenda kisimani ukateke maji." Wote wawili wakaenda. Sadiki alinunua samaki, akarudi nyumbani haraka. Lakini Sikiri alichelewa. Baba yake akamngoja mpaka akachoka.

Baba akatoka kwa hasira kumfuata Sikiri kule kisimani. Alipofika alimkuta anachezea maji. Anayateka na kuyamwaga juu ya jiwe. Baba yake akamwuliza, "Unafanya nini Sikiri? Mbona unacheza tu? Teka maji, twende nyumbani." Sikiri akateka maji, wakarudi nyumbani.

Walipofika nyumbani walimkuta mama amekwisha tayarisha uji. Wakanywa. Walipomaliza, baba yao akawaambia, "Twendeni tukapalilie bustani ya mboga. Mama atabaki hapa nyumbani. Atalisha kuku na kusafisha nyumba. Baadaye atatayarisha chakula."

Kule katika bustani kulipandwa mchicha, maharagwe, vitunguu na nyanya. Magugu na manyasi yaliota kwa wingi. Sadiki, Sikiri na baba yao walipalilia kwa uangalifu ili wasiharibu mimea ya mazao.
Sikiri hakupenda kazi. Kwa hiyo alitoroka akaenda
kichakani. Kule kichakani alitafuta matunda mwitu. Sikiri alikuwa mtoto mvivu kweli. Hakutaka kufanya kazi kwa bidii. Sadiki na baba yake waliporudi nyumbani, akawafuata.

Walipofika nyumbani chakula kilikuwa tayari. Sikiri alikuwa wa kwanza kunawa mikono na kuanza kula. Siku ile mama alipika ugali na samaki alionunua Sadiki. Walipokwisha kula, baba alimwita Sikiri akamwuliza, "kwa nini leo alitoroka?" Sikiri alinyamaza tu. Sakiri alikuwa mtoto mkaidi. Baba akamwambia, "Kesho utakwenda kupalilia bustani. Usipokwenda hutapata chakula."

Siku iliyofuata Sikiri alikataa kwenda bustanini, alitoroka. Sadiki na baba yake walikwenda kupalilia peke yao. Jioni waliporudi, baba alimwuliza mama, "Sikiri amekwenda wapi?" Mama akajibu, "Mimi leo sijamwona nyumbani. Sijui amekwenda wapi." Kumbe, siku ile asubuhi Sikiri alipanda basi kwenda mjini Kigoma. Huko njiani aliulizawa nauli .

Sikiri hakuwa na pesa hata kidogo. Dereva akamtelemsha pale pale. Akaachwa peke yake. Sikiri alilia sana . Mwisho akaanza kusema kwa uchungu:-

Sikiri mimi maskini,
Uvivu wangu nyumbani,
Ukiwa huu njiani,
Nakufa hapa kwa nini?

Sadiki sasa ashiba,
Chakula kingi kwa baba,
Nirudi tena kwa baba,
Nakufa hapa kwa nini?

Sikiri alirudi nyumbani. Alikuwa amechoka sana. Alipofika nyumbani aliomba radhi. akamwambia baba na mama.


Naomba radhi nimekosa,
Nitakuwa mtoto mwema sasa,
Shambani tena sitakosa,
Baba na mama nisameheni .

Nitalima kama Sadiki,
Nitalima wala sichoki,
Na nyumbani tena sitoki
Baba na mama nisameheni.

Baba hakumpiga Sikiri. Alimsamehe. Sikiri akabadili tabia yake, akawa anawasaidia wazee wake. Kila alipotumwa alikwenda upesi. Mama yake alifurahi, akamwambia,

"Siku hizi wewe ni mtoto mwema kama Sadiki. Mtoto mtii hupendwa na wazazi wake. Tena hupendwa na watu wote kijijini. Endelea kuwa mtoto mwema na mtii.


......MWISHO......












**VITABU:**

**Jipatie vitabu pendwa vya riwaya tamu za kijasusi. MPATANISHI na HARUFU YA KIFO kutoka Jamvi la Simulizi. Vilivyoandikwa na mwandishi wako wa siku zote ambaye hana maneno mengi ila kalamu yake itakuonesha ubora wake.**

**Wahi sasa katika sehemu elekezwa ili ujipatie chako.**

**MPATANISHI—12,000/= na HARUFU YA KIFO—12,000/=**

**Aidha tunauza nakala laini ya vitabu mbalimbali vya riwaya za kijasusi. Usiwe mpweke, fanya uwezalo ukamate nakala yako.**









# SHUBAKA LA VITABU

**NAMNA GANI UTUNZE VITABU VYAKO VIDUMUKWA MUDA MREFU**

**Leo katika safu yetu ya Shubaka la Vitabu tunakuja na jambo hili la utunzaji wa vitabu. Katika matoleo yaliyopita tuliweza kuhojiana na wasomaji na wapenzi wa vitabu ili kujua namna wanavyothamini na kutunza vitabu vyao. Sasa basi leo tunakufunda katika hilo.**

**Na: Richard Mwambe**

Kwa mtu anayependa kusoma, mara nyingi huwa na maktaba yake binafsi nyumbani. Kadiri maktaba yako ya nyumbani inavyokua, unaweza kuwa unatafuta jinsi gani ya kuhifadhi vizuri baadhi ya vitabu vyako ili vitunzwe kwa usalama kama vitu vingine vya nyumbani. Lakini, lazima ujue kuwa vitabu ni nyeti sana, na visipohifadhiwa vizuri hali yake inaweza kuwa mbaya. Je, unajua jinsi ya kuhifadhi vitabu vyako kwenye kifaa cha kuhifadhi? Soma safu hii kwa vidokezo muhimu vya jinsi ya kuhifadhi vitabu katika uhifadhi wa muda mrefu.

**MAMBO 6 YA KUZINGATIA UNAPOHIFADHI VITABU**

**1—Linda vitabu vyako dhidi ya vyakula na maji**

Kwanza kabisa hautakiwi kula au kunywa wakati wa kusoma. Elewa kwamba mabaki ya chakula yaliyoachwa mezani yanaweza kuharibu kitabu. Ukiweka kitabu kwenye sehemu ambayo imeathiriwa na chakula, maji au unyevunyevu unaweza kutokea na kuenea katika kitabu chako. Ili kuzuia vitabu vyako visiharibike, hakikisha kuwa ni safi kabla ya kuhifadhi. Usile wakati unasoma na weka mbali vitabu na meza ya chakula

**2– Funga kitabu kwa umakini ukitumia kitambaa**

Kabla ya kuweka vitabu vyako au vitu vyovyote vya nyumbani kwenye hifadhi ya muda mrefu, vifunge kwa taulo za karatasi au kitambaa. Hii itasaidia kuvilinda kutokana na uharibifu wowote unaosababishwa na uchafu au vumbi.

**3– Tumia chombo kutunza vitabu**

Tunapendekeza kuhifadhi vitabu kwenye chombo cha plastiki au malighafi yoyote ngumu. Hii itasaidia kulinda zaidi vitabu vyako dhidi ya unyevu, vumbi na wadudu waharibifu kama mchwa.

**4– Hifadhi vitabu vyako kwa wima**


Unapoweka vitabu vyako kwenye chombo cha kuhifadhia au rafu viweke katika mtindo wa wima huku kingo za karatasi zikitazama juu. Njia hii husaidia kulinda umbo la vitabu kwa kuruhusu vitabu kusaidiana. Kuwa mwangalifu usijaze vitabu vingi kwenye kisanduku kimoja, kwani inaweza kusababisha migongo ya vitabu kupinda.

**5—Tumia chombo cha kuhifadia kinachodhibiti mabadiliko ya na hali ya hewa kwa uhifadhi wa Muda Mrefu**

Mojawapo ya njia bora za kuhifadhi ubora wa vitabu vyako ni kuvihifadhi katika chombo chenye uwezo wa kudhibiti hali ya hewa. Chombo cha namna hiyo kitaweza kitadumisha halijoto anuai ambayo ni bora kwa kuhifadhi vitu nyeti zaidi kama vitabu.

**6— Angalia Vitabu Vyako**

Jambo baya zaidi unaweza kufanya wakati wa kuhifadhi vitu nyeti kama vitabu ni kuviweka kwenye hifadhi ya muda mrefu na kuvisahau. Weka kikumbusho kwenye simu yako au saa yako ili uangalie vitabu vyako . Ikiwa kuna uharibifu, utahitaji kushughulikia mara moja ili kulinda mkusanyiko wako



# KITABU NILICHOSOMA




## KOVU LA MOYO – 02

**Anaandika Joynice Joseph**

MWANDISHI wa kitabu ni Mariam Mbano.

Kovu la moyo ni kitabu ambacho nimekua nikivutiwa kukisoma Mara mbilimbili,na wala sihishiwi hamu kukisoma tena na tena kwa jinsi kilivyo na madini ya kutosha ndani yake.

Kovu La Moyo kinamulika uhalisia wa maisha tunayoishi kila siku katika uhusiano wa kimapenzi, binafsi nimejifunza mambo mengi sana, tena kimenifanya niweze kuyakabili na kuyamiliki maisha yangu.

Mwandishi ameelezea namna bora ya kuboresha mawasiliano kwa wapendanao, pia kujijua wewe binafsi na uhusiano ulionao

1.Uhusiano unajengwa na pande mbili, yaani upande wa mwanamke na upande wa mwanaume, kila upande unapaswa kushiriki katika kuujenga uhusiano, ili mahusiano yaweze kua imara,na yenye upendo wa dhati. (Uhusiano ambao unaelemea upande mmoja, huwa hauchukui *round* kuvunjika hata kufikia kikomo. Mara tu yule ambaye alikua anajenga akichoka basi uhusiano unaishia hapo)

2.Ni muhimu kujadiliana kwa kina, *once* mnapoingia katika mahusiano, kuhusu ndoto na malengo yenu, ili kuangalia namna bora ya kuyatimiza, bila kuathiri lengo la mmoja wenu. Mfano kwenye simulizi ya George na Getrude katika kitabu, kila mmoja alikua ana malengo tofauti na mwenzake, Getrude ana biashara ya nguo Dsm huku mpenzi wake anawaza kuwekeza Mbeya awe mkulima mkubwa. Kutofautiana kwa malengo kunaweza kuua kabisa mahusiano, kama George alivyoachana na Getrude.

3.Kujua lugha za mapenzi ambazo mwenza wako anazungumza. Ili uweze kuboresha na kuimarisha uhusiano wenu, Jua mwenza wako nini anapenda kufanyiwa na kipi hapendi, ili kutoziua hisia za mapenzi kati yenu,

Mwandishi ameelezea kitabu Cha *THE 5 LOVE LANGUAGE* By Gary Chapman, kinaonyesha lugha za



mapenzi zipo 5; kama vile kupeana zawadi, kusaidiana kazi nk,

6.Kuzimudu/kuzikabili hisia, kutolipa visasi au kutofanya visa, vurugu, vibwanga na mikasa kwa *ex* wako, kisa tu umeachwa/au mmeachana. Mfano vile Getrude alivyomuandama *bae* mpya wa *ex* wake(Beatrice) hata akafikia hatua ya kumtumia majambazi ili wamzuru.

Na siajabu ndomana George alimwacha kwakua alikua hawezi kujizuia/kukabiliana na hisia zake.

7. Mambo ya kufanya pale penzi lenu linapofika tamati, Tengeneza mfumo mpya wa maisha, achana kabisa kutaka kujua habari za *ex* wako hazitakusaidia chochote zaidi ya kukuumiza, *focus* kwenye maisha yako, timiza malengo yako, usikae kizembe fanya shughuli za kukuingizia kipato, lia maliza, vaa pendeza kua *smart* endelea kujipenda kuwa mtu mwenye furaha,hii itavutia hata watu sahihi kukupenda tena.

Tofauti ukijichukia na kujiacha rafu ukawa mtu wa kulialia tu, hata watu hawawez kukupenda tena mana hujatambua thamani yako. Kovu la moyo kimeeleza jinsi ya kutambua thamani yako.

8.Jipe muda wa kupumzika, Jitulize, usikurupuke, umetoka kuachwa, kuacha, au kuachana leo kesho ushaanza mahusiano mapya, *Big* noo, kitabu kinaeleza namna ya kujipa muda, pumzika, tumia huo muda kutafakari mahusiano yako yalopita. Basi yale madhaifu yako yafanyie kazi, ni vyema kupumzika atleast *3 up to 6 month* ndipo uanze mahusiano mapya, hata akili nayo itakua imer*elax*,l akin usipojipa muda basi unakua mtu ambaye unamahusiano yasiyodumu, mana haujipi muda wa tathmini.

9.Usirudiane na mtu kwasababu unampenda, mapenzi pekee hayafanyi uhusiano kua Bora, kitabu kinaelezea mambo ya kuzingatia pale unapotaka kurudiana na *ex* wako, na mambo ya kuzingatia kabla hujafanya uamuzi huo, pamoja na mbinu za kurudiana na mpenzi mliyeachana .

Mfano simulizi ya Florida na Sweetbert jinsi walivyorudiana.

***R.M***

# Tangazo

**Ile App ya Jamvi la Simulizi uliyokuwa ukiisubiri kwa hamu sasa ipo tayari, ipo Playstore kwa wale wote watumiaji wa Android. Ipakue sasa ujisomee riwaya ya Kamanda Amata bure, majarida ya Ngurumo ya Mwandishi matoleo yote na picha za matukio mbalimbali. Kwanini ujitenge? Jiunge na familia kubwa ya Jamvi la Simulizi.**

**Jinsi ya kufanya:-**

**Fungua simu yako, chagua Play Store > kwenye search andika 'Jamvi la Simulizi'> kisha bofya Download/Install > Open**

**Ikishafunguka basi ingiza email yako na password… tayari utakuwa umejiunga. Njoo tufurahi pamoja.**










---

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com